# **TATHIMIN** YA VVU NA UKIMWI

# TAHTHIMIN Inaendelea

- Ukimwi unazidi kuenea duniani kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na shirika la (UNAIDS mwaka 2012) inakadiriwa watu million 34 ulimwenguni wanaishi na virusi vya Ukimwi zaidi ya hapo mwanzo.
- Hii inasababishwa na matumizi ya dawa za kurefusha maisha ARVs

# THATHIMIN Inaendelea

- Nchi zilizo chini ya jangwa la sahara ikiwemo Tanzania zimeathirika sana na jangwa hili, kwa  mwaka 2011, inakadiriwa kuwa million 1.8 sawa na 69% ya maambukizi mapya yalipatikana katika nchi zilizochini ya jangwa la sahara

# TAHTHIMIN Inaendelea

- Nchini Tanzania ugonjwa wa Ukimwi ulianza mwaka 1983 ili ripotiwa kuwa wagonjwa watatu wamepatikana mkoani Kagera na ilipofika mwaka 1986 mikoa yote ili ripotiwa kupata maambukizi.
- **Kwa sasa takwimu zinaonyesha watu milioni 1.5 wanaishi na virusi vya UKIMWI kati ya hao 28% ni watoto wa umri wa miaka 0-14. na 11.2% ni kati ya umri wa miaka 15- 24**
- UKIMWI umechangia ongezeko la idadi ya watoto yatima nchini, Vilevile UKIMWI umechangia kupunguza kiwango cha matumaini ya kuishi kutoka umri wa miaka 62 mwaka 1992 hadi miaka 48 mwaka 2003.

# THATHIMIN Inaendelea

- Kuanzia mwaka 2004-2008, maambukizi ya ukimwi nchini Tanzania yamepungua kutoka asilimia 7% mpaka asilimia 6%
- Kutokana na ripoti ya mwaka 2011 inakadiriwa watu 1.6 milioni nchini Tanzania wanaishi na virusi vya ukimwi, kati yao milioni 1.3 ni wenye umri wa miaka 15 na kuendelea (ripoti ya UNAIDS)
- Na thamini ya mwaka 2012 inaonyeshakuwa kiwango cha maambukizi ya ukimwi kimepungua kutoka asilimia 6% mpaka asilimia 5.1%

# HALI HALISI YA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA UKIMWI MKOANI

- Mkoani Geita kutokana na ripoti ya mwaka 2011-2012 kiwango cha watu walioathirika na Ukimwi ni 4.7% kwa umri kati ya miaka 15-49.

# HALI HALISI YA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA UKIMWI WILAYANI

- Mwaka 2010, jumla ya watu 43,124 walipima virusi vya ukimwi kati ya hao 2,764 walikuwa na maambukizi ya virusi vya UKIMWI (6.4% )
- Aidha, Mwaka 2011 jumla ya watu 168,991 walipima virusi vya ukimwi kati ya hao jumla 11,286 walikuwa na maambukizi ya virusi vya ukimwi (6.6%).

# inaendelea

- kwa sasa (2015) takwimu za maambukizi zinaonyesha kupungua hadi kufika 4.9%.
- Na hii inachangiwa na elimu ya mapambano dhidi ya VVU kuwafikia vizuri wananchi.

# *Hali halisi ya maambukizi katika Wilaya: Inaendelea*

- **Wanaume:**
- Jumla ya watu **6,055** walio kati ya miaka **15-24** walipima virusi vya ukimwi,kati yao jumla ya watu **56** sawa na **(0.9%)** walikutwa na maambukizi ya virusi vya ukimwi.
- Jumla ya watu **2,363** walio kati ya miaka **25-49** walipima virusi vya ukimwi,kati yao jumla ya watu 273 sawa na (**11.6%)** walikutwa na maambukizi ya virusi vya ukimwi
- Jumla ya watu **508** walio zaidi ya miaka **50** walipima virusi vya ukimwi kati ya hao jumla ya watu **41** sawa na **(8.1%)** walikutwa na maambukizi ya ukimwi.

# Hali halisi ya maambukizi katika Wilaya :Inaendelea

- Wanawake:
  - Jumla ya watu 637 walio kati ya miaka 15-24 walipima virusi vya ukimwi ,kati ya hao jumla ya watu 66 sawa na (10.4%) walikuwa wameambukizwa virusi vya ukimwi.
  - Jumla ya watu 1,049 walio kati ya miaka 25-49 walipima virusi vya ukimwi ,kati ya hao jumla ya watu 248 sawa na (10.4%) walikuwa wameambukizwa virusi

# MADA VIJANA

- COPY

MADA : 2WAJIBU /MAJUKUMU YA HALMASHAURI DHIDI YA MAPAMBANO YA UKIMWI

- Utangulizi :

Serikari kwa kushirikiana na wadau wanaowajibu na majukumu mbalimbali ikiwa ni moja ya kutekeleza sera ya taifa ya kudhibiti ukimwi

Ukimwi umekuwa ni suala mtambuka ambapo kila sekta na shughuli zote za kitaifa lazima lipewe kipaumbele katika mapambano hayo.

Sera hii inawajibisha kila sekta kuandaa na kutekeleza mipango ifaayo ya kuzuia kuenea kwa VVU/Ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa,kukinga na kusaidia makundi yaliyoathirika na kupunguza athari za kiuchumi na kijamii.

# WAJIBU WA HALMASAHURI KAMA MDAU

- Kuelimisha makundi mbalimbali ya jamii juu ya janga dhidi ya magonjwa ya ngono na virusi vya ukimwi.
- Kuhakikisha usalama wa damu n aviungo vya mwili pamoja na kusisitiza matumizi ya bomba moja la sindano kwa mtu mmoja.
- Kuhakikisha elimu ya kondomu na kondomu bora zinapatikana kwa bei nafuu maeneo yote ya wilaya .

*Wajibu unaendelea*

- Kuchukua hatua madhubuti kuzuia maambukizi kutoka kwa Mama kwenda kwa mtoto(kabla ya kujifungua,wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua).
- Kupima virusi vya ukimwi _kuhakikisha vifaa vya kupimia vinapatikan muda wote na wakati wa sherehe za kitaifa- i.e mwenge.
- Kutoa huduma kwa watu wanaoishi na virusi vya ukimwi na wenye ukimwi – Lishe bora na ushauri nasaha ,kuzuia na kupunguza unyanyapaa.

# Wajibu unaendelea

- Kushirikishi jamii kwenye mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya ukimwi ikiwa ni kutambua maeneo hatarishi –i.e machimboni,maeneo yaliyo kando ya lami.
- Kulinda haki za watu wanaoishi na virusi vya ukimwi ili kuinua ubora wa maisha yao n akupunguza fedheha,kwa kuwapatia dawa za kurefusha maisha (ARVS)
- Kushirikiana na wadau katika kuhakikisha jamii inaelimishwa kuhusu umuhimu wa kujikinga dhidi ya magonjwa ya ngano kupima na kutibiwa mapema magonjwa hayo

# Wajibu unaendelea

- Kusaidia watoto yatima ,walio katika mazingira magumu na watoto wasiojiweza kuwalipia ada.
- Kusimamia vikao vya kamati ya kudhibiti ukimwi ngazi ya wilaya (CMAC) na idara mbalimbali zinatoa huduma ya chakula cha lishe kwa watumishi walioathirika.